BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

OROFDHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA TISA

Kikao cha Kumi na Nne – Tarehe 22 Mei, 2025
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka 2025/2026.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka 2025/2026.

## III. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

265. MHESHIMIWA BAHATI KHAMIS KOMBO (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Je, kuna utaratibu gani wa Serikali wa kuwapandisha madaraja watumishi wa Serikali ambao tayari wameshafanya kazi zaidi ya miaka saba.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

300. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Je, ni kiasi gani cha fedha kimetolewa kwa vikundi vya vijana, kinamama na watu wenye mahitaji maalum wa jimbo la Wawi katika programu ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

234. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kumekuwa na malalamiko kwamba baadhi ya Serikali za Mitaa hushindwa kuchangia kikamilifu asilimia kumi ya mapato yanayotokana na makusanyo yao ya ndani kama ilivyoelekezwa na Sheria Namba 7 ya mwaka 2014.

(a) Je, suala hili linafahamika vipi na Wizara yako.

(b) Je, ni sababu gani zinazopelekea kushindwa kutekelezwa matakwa ya Sheria Namba 7 ya mwaka 2014.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

29. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Tokea Serikali kuanza mchakato wa kutoza $44 kwa kila mgeni anaeingia Zanzibar, mchakato huo umeleta changamoto na malalamiko makubwa kwa nchi za Jumuiya ya Africa Mashariki (EAC), kwakuwa lengo la EAC ni kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi, kijamii na kisiasa miongoni mwa nchi wanachama kwa lengo la kuboresha ustawi wa wananchi.

(a) Je, ni kwa kiwango gani Serikali inaitambua changamoto hii kwa wananchi wa EAC wanaoingia Zanzibar.

(b) Je, ni zipi juhudi za Serikali za kuhakikisha kwamba haiendi kinyume na makubaliano ya EAC katika kadhia hii.

(c) Je, ni ipi tathmini ya uingiaji wa wananchi wa Jumuiya ya Africa Mashariki kwa kipindi cha Oktoba, 2024 hadi Februari, 2025.

**<u>Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:</u>**

124. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

 Hamasa ya kujiunga na vikundi vya mazoezi ndani ya jimbo la Mwanakwerekwe imekuwa kubwa kuanzia rika la vijana, wanawake na wazee.

 Mheshimiwa Waziri, je ni lini utavitembelea kwa utaratibu maalumu vikundi hivi ili kuwafariji na ikibidi kutatua baadhi ya changamoto zinazowakabili.

**<u>Wizara ya Afya:</u>**

185. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

 Ni mageuzi gani makubwa tunaweza kujivunia katika mageuzi ya sekta ya afya ikiwa ni mchango mkubwa wa azma njema ya Mhe. Rais.

**<u>Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:</u>**

212. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

 Ni lini ahadi yako ya kukipatia vifaa visaidizi vya kufundishia Chuo cha Ujasiriamali cha Vijana, jimbo la Mwanakwerekwe itakamilika kwa usahihi wake.

**<u>Wizara ya Maji, Nishati na Madini:</u>**

263. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

 Natambua juhudi kubwa zinazofanyika katika kupunguza changamoto ya maji nchini. Hata hivyo, bado changamoto hii inaendelea kuwakabili wananchi katika baadhi ya maeneo.

 Je, ni upi mkakati wa Serikali wa kukabiliana na changamoto hii.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

164. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Licha ya jitihada za viongozi wa jimbo kujenga baadhi ya vivuko na vidaraja, bado baadhi ya maeneo yanahitaji huduma hizi kwa kiwango kikubwa.

Ni lini Wizara itafanya marekebisho na kulijenga daraja la Magogoni Kidatu kuelekea kwa Mwarabu, ili kuwaondolea usumbufu wananchi na kuwawezesha kupita wao na mali zao.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

123. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

(a) Ni lini Wizara yako itafanya ziara na kuwatembelea wakulima wa mboga mboga ndani ya jimbo la Mwanakwerekwe kwa lengo la kuwaendeleza kitaaluma na kuwapatia mipango ya uwezeshaji.

(b) Kwa kuwa wapo Wazee Wastaafu jimboni Mwanakwerekwe walioanzisha kilimo cha mboga mboga ili kujiendeleza, je, Wizara yako ipo tayari vipi kuwaona na kuwapatia wataalamu stahiki pamoja na pembejeo muhimu za kuendeleza kilimo hiki cha mboga mboga.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

147. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

'Botanic Garden' ni maeneo yenye kubeba kumbukumbu na kuhifadhi aina mbali mbali za miti na mimea adimu.

Ni aina gani za kumbukumbu na miti adimu iliyobakia kwa sasa katika eneo la 'Botanic Garden' iliyopo Kilimani mjini Zanzibar.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

### Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa mwaka 2025/2026.

### Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka 2025/2026.

**Zanzibar,**
**22 Mei, 2025.**

**(Raya Issa Msellem)**
KATIBU WA BARAZA LA
WAWAKILISHI, ZANZIBAR